**KAZI YA ZIADA**
**KISWAHILI**
**GREDI YA 8 2024**

**JINA: ………………………………………………………………………………………**
**SHULE: ……………………………………………………………………………………**
**NAMBA YA MTIHANI………………………………………TAREHE: ……………………….**

**INSHA**

Kutakuwa na tamasha itakayoshirikisha michezo ya kuigiza, nyimbo n amashairikutoka shule mbalimbali katika kaunti yenu. Andika ratoba ya siku hiyo. (Alama 20)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali***

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili yamahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na. matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!" Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima." Hata Marekani na ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha

demokrasia. Chini walilaliana kama Vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka. Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya ‘ mkereketwa wa Uafrika akachanganua.

Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagikaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutaruta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati. Hali hil imesababisha maafa makubwa, uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa ainati, uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali. Huku mataifa mengi Ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali‘ Tutaendelea vipi na tunadhulimiwa na kaka wakubwa”. Siasa ya demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ulitima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambayo hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora, uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii uliosisiwa na Jean Jacques Rousseau.

**Maswali**

a) Binadamu amechanganyika kwa njia ipi? (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

b) Ni vipi Demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

c) Kwa nini inasemekana kuwa ‘Demokrasia ni mchezo wa mizengwe? (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

d) Ni athari gani hutokana na kinyang’anyiro cha Demokrasia? (Alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

………………………………………………

e) "Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi-hewa wa wanasiasa" Eleza. (Alama2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

f) Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yalivyotumika katika taarifa. (Alama 3)

i) Mafahali

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………Wanatupikia majungu

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………Ukarabati

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

1. **MATUMIZI YA LUGHA.(Alama 30)**

a) Taja kikwamizo hafifu cha ufizi. (Al 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Tambua aina za vitenzi katika sentensi hii. (Al 2)

Wale waliokuwa hapa sio wageni wetu.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

c) Alama ya Nukta mbili huweza kutumika kuorodhesaha vitu. Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha namna alama hiyo inaweza kutumiaka. (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

d) Yakinisha sentensi ifuatayo . (Al 2 )

Usipopita mtihani hutakuwa shujaa mapema.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

e) Sahihisha sentensi hii kwa njia mbili mwafaka. (Al 2)

Dereva ambaye aendeshaye kwa uangalifu husalimika.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

f) Tunga sentensi sahihi huku ukitumia kihusishi cha wakati. (Al 1)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

g) Ainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (Al 3)

Mwanafunzi mtundu ameadhibiwa vikali na mwalimu.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

h) Eleza ‘po’ ilivyotumika katika sentensi hizi. (Al2)

Alipofika waliposimama, waliondoka.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

i) Tumia kiunganishi kifaacho kuunganisha sentensi hii. (Al 2)
Juma hakusoma kwa bidii. Amefuzu mtihani.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

j) Geuza sentensi hii iwe katika usemi wa taarifa. (Al 3)
" Nimekuwa nikija kwenu kila siku lakini nimeamua kulikata guu langu," Hamisi akamweleza Amina.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

k) Andika sentensi hii kwa ukubwa. (Al. 1)
Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

l) Eleza matumizi ya " KI" iliyopigiwa mstari katika sentensi hii. (al 3)
U<u>ki</u>rusha <u>ki</u>pira hiki <u>ki</u>tapotea.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

m) Andika maana tatu zitokanazo na sentensi hii. (Al 2)
Mama alimpigia mtoto mpira.

.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………………………………

n) Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya vitate vifuatavyo. (Al 2)

i) Chaka

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

ii) Shaka

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kiwakilishi kisisitizi cha mbali kidogo ngeli A- wa katika hali ya wingi . (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

**2. <u>FASIHI SIMULIZI (Alama 5)</u>**

a) Eleza maana ya vitanza ndimi. (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

b) Eleza umuhimu wa jamii kutumia vitanza ndimi. (Al 3)

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

3. **ISIMU JAMII (Alama 5)**

**Ali:** Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!
**Ebo:** Mimi……ni….afande ni Ebo
**Ali:** Unatoka wapi saa hii? Hapa hakuna sheria?
**Ebo:** Samahani mkubwa. Mimi niku……
**Ali:** Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini
**Ebo:** pole mzee
**Ali:** Mzee gani? Hii mtu lazima niiweklw store. Yaani Self contained. Toa viatu.
**Ebo:** Tafathali Bwana Askari, nilichelewa…..
**Ali:** Mimi sitaki hadithi. Hizo pelekea nyanya yake,eh. Fanya haraka!
**Ebo:** Naomba mkubwa…..
**Ali:** Hapa si kanisani. Unaomba! Hata…….

a) Fafanua sifa tano za sajili hii. (al 5)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………